# AINA KUU TATU ZA WATU
# MAANDIKO: 1KOR. 2:14 – 15

1. **UTANGULIZI**
   Maandiko ya Neno la Mungu kimsingi kabisa yanawagawa wanadamu wote katika matabaka makuu matatu.

a. **Tabaka la kwanza ni lile la mtu wa asili- 1Kor. 2:14** (au tuite mtu asiye wa kiroho!!! Huyu ni mtu ambaye hajafanywa upya, ni mtu ambaye anaendelea kutawaliwa na hisia zake za asili (macho, pua, masikio, ulimi na kupapasa (mikono), hawa ni watu ambao hawana Roho Mtakatifu na kwa asilimia mia moja wako chini ya utawala wa shetani. ***Mdo. 26: 12 – 18;*** Hawa ni watu ambao kamwe hawamjui Mungu na njia zake na muda wao wote wanaishi kwa kuzitegemea akili zao (ufahamu wao na hisia za kibinadamu. Ni wana wa Adamu wa kwanza. ***1Kor. 15: 45 - 49.*** Yesu aliwaita kuwa ni wana wa ibilisi (Baba yao ni ibilisi) **Yoh. 8:44, Mdo. 13:10**

***b.*** **Tabaka la pili ni lile la mtu wa kiroho** .***1Kor. 2: 15, 3:1.*** Hawa ni wanadmau wote waliofanywa upya na Roho Mtakatifu baada ya kumkiri nakumpokea Bwana Yesu kuwa Bwana na Mwokozi wao(Paulo anawaita kuwa ni watu wa (Rohoni) kwa sababu wanakuwa ni watu wanaoishi kwa kufuata uongozi wa Roho Mtakatifu; hawaendeshwi tena na tamaa za miili yao na dhambi inakuwa haina mamlaka tena juu yao**.** ***Rum. 8:13 - 14, 1Kor. 2: 6 –13, Gal. 5: 16 – 18, 2Kor. 5: 16 – 17, 1Yoh. 5: 10 – 12.*** Kwa jina lao wanaitwa wanawa Mungu**.** ***Yoh. 1: 12 – 13, 1Yoh. 3: 10.***

**Note:** Mtu anakuwa wa Rohoni pale tu anapompokea Yesu Kristo kuwa Bwana na Mwokozi wake; saa hiyo hiyo Roho Mtakatifu humuhuisha na kuweka ndani yake upya wa uzima unaotoka kwa Mungu na anabadilishwa ufahamu wake na mtazamo wake na anaanza kuishi maisha ya utakatifu hapa duniani na kushangaza wengi waliomfahamu huko nyuma. ***Mdo. 9:19- 22, 26-31, Efeso 2: 1 – 10, 1Kor. 15: 48.***

- Na Roho Mtakatifu saa zote anakuwa na kazi maalumu ndani ya mtu huyu wa rohoni ya **kumfunua Yesu Kristo ndani yake pamoja na uzuri wake** jambo ambalo litamfanya hata akipitia changamoto za aina mbalimbali za maisha haya,

**asimame** bila kubabaika wala kukata tamaa kabisa. Yaani Roho Mtakatifu ndani ya mtu huyo **anamwezesha** kuishi maisha ya aina zote na kuchukuliana na hali zote ngumu au za mafanikio atakazokutana nazo katika safari hii bila kutenda dhambi tena. **Filip. 4: 10 - 13. Hawa ndiyo walio na sura halisi ya Kristo Yesu katika maisha yao ya sasa hapa duniani, na muda wote wanakuwa adui kwa shetani na majeshi yake.**

***c.*** **Tabaka la tatu ni lile la Wakristo wa Kidunia. (Tabaka la watu walio na mfano wa utauwa) 1Yoh.2: 15 – 16, 2Tim. 3: 5, hawa ndiyo Bwana Yesu aliwaita kuwa ni mbwa mwitu wakali walio na mfano wa kondoo kwa nje lakini kwa ndani ni mbwa mwitu wakali. Math. 7: 15-16.** Hili ni kundi la watu wanaojiita Wakristo lakini linaishi bila kujali sheria za Mungu (ni kundi lenye kuasi kila siku sheria za Mungu na kufanya linayoyataka lenyewe ingawa limevaa jina la Ukristo-kundi la watu vuguvugu.***Ufun.3:14-17***

- Biblia inaposema "**msiipende dunia wala mambo yaliyomo katika dunia (kosmos**) inamaanisha hasa **MIFUMO.**

- Shetani ameiweka dunia katika mifumo mibaya inayopingana na sheria za Mungu. Sasa hivi ukifuatilia kwa makini sana; nyuma ya kila shughuli zote za kibinadamu, kuna nguvu fulani ya ibilisi inayotenda kazi kwa siri sana, iko roho inayotenda kazi nyuma yake iliyo kinyume kabisa na Mungu pamoja na Neno lake!! Na ndiyo sababu shetani anaitwa Mungu wa dunia hii. **Yoh. 14:30, Yoh. 12: 31 (mfano – angalia mifumo ya udaktari, Serikali nyingi leo, tamaduni nyingi (mavazi) hata mifumo ya elimu leo (sayansi), mifumo ya muziki, mifumo ya uchumi, mifumo ya vyombo vya habari, mifumo ya dini, mifumo ya michezo mingi!! mifumo ya siasa nyingi n.k. karibu yote inapingana na Mungu aliye hai na sheria zake (Neno lake)** na ndiyo sababu Yohana anawaonya watoto wa Mungu wasiipende dunia wala mambo yaliyomo katika dunia.

- Haikanushiki kabisa kwamba shetani ndiye Mungu wa mifumo ya sasa ya Ulimwengu huu pamoja na majeshi ya pepo wabaya na ndiyo wanaotawala na kuendesha Ulimwengu huu. ***Yoh. 12: 31, 14: 30, 2Kor.4: 3 – 4.***

- Chukua mifano ya dini nyingi ambazo zinamtaja Yesu kwa kinywa lakini hapo hapo zinakana mafundisho yake hadharani!!! Ndiyo sababu kuna umuhimu wa wateule kuishi kwa kujilinda sana na kuwa na taadhari ya hali ya juu ili wasijikute wamenaswa. ***1Yoh. 5: 18.***

***Note:*** **Mtume Yohana ameonya sana Wana wa Mungu wasipende dunia katika maeneo makuu matatu.**

a. **Wajiepushe na tamaa ya mwili** – yaani wajiepushe na kukimbilia **anasa** za dhambi (**mwili kama mwili kuna mambo unayatamani daima kama zinaa, kula kwa anasa, kuvaa kwa anasa (splendor) fahari, utukufu, (haya ndiyo mambo mwili unataka!!! Na ndiyo yaliyoko duniani kote kwa sasa. Luk. 16: 19*. (zinaa, anasa, fahari, utukufu (waheshimiwa).**

b. **Wajiepushe na tamaa ya macho** – Hii maana yake hasa ni kujiepusha na kutazama vitu vinavyovutia macho yako ambavyo Mungu amekukataza usivitazame. ***Mwanz. 3: 6,*** **Yosh. 7: 20 – 21 (Kut. 20:17)** ona hata Mfalme Daudi na tamaa ya macho – ***2Samwl. 11: 2-5.***

- **Tunapowaonya wateule juu ya kutazama picha mbaya za ngono, mauaji, ukatili, maonyesho ya kimila yasiyo na staha, kusoma magazeti/vitabu vya hovyo n.k. ni kwa sababu Biblia inajua athari zake na kutuonya mapema. Math. 5: 27 - 29, Ayub. 31: 1, lakini bado watu wa Mungu wanavutiwa tu kuangalia, kusoma na kujadiliana na mambo haya kwa kudhania kwamba wao ni werevu kuliko Neno la Mungu.**

c. **Wajiepushe na kiburi cha uzima** – wajiepushe na kujisifu sifu kutokana na yale ambayo wameyatenda baada ya kuokoka au kutokana na karama **walizonazo (watu waache kujigambagamba) kawaida roho ya kujiinua na kutafuta kujitukuza** na **kujitangaza** haitokani na Mungu!! ***Yer. 9: 23-24, 50: Yak. 4:13 -16, Efes. 2: 8-9, 2Kor.12: 1- 5, na Waam. 16: 4 – 20*.20.***

***Note:*** Wakati adui za Samsoni wanatafuta kujua asili ya nguvu zake nyingi alizonazo; yeye Samsoni badala ya kutafuta pia siri ya ushirika wa karibu mno na Mungu aliye asili ya nguvu zake nyingi, anabakia na mazoea na kujisifu pamoja na kujigamba!! **alijaa sana Samsoni kiburi cha uzima. Anasema**

**nitakwenda kupigana kama kawaida yangu. Mst. 20 (*I will wake up and shake myself)***

- **Kilichompumbaza Samsoni zaidi pale alipokutana na Delila ni kwa sababu Delila alizaliwa na Baba Mfilisti na Mama Myahudi, Delila akafahamu, lugha ya Kiyahudi kwa ufasaha sana; na alipoajiriwa na Jeshi la wafilisti kama askari wa kulipwa (jasusi), Delila aliongea na Samsoni muda wake wote lugha ya Kiyahudi kiasi Samson alipumbazika na kutoboa siri na kuwa ndiyo mwisho wa huduma yake. Delila hakumpenda Samsoni kamwe; bali alikuwa kazini bila ya Samsoni kujua. Rum.16: 18; Delila alivaa vazi la upendo wa bandia wakati ndani yake ni mbwa mwitu mkali mno kwa Samsoni.**

**"Ona adui anavyosema hata kwako na kwanguleo"Waam.16:4– 5."** Huu ndiyo mfumo wa dunia hii kwa kila mwana wa Mungu halisi; dunia haitupendi ng'oo hata kama inatuchekea, inatafuta nafasi usiku na mchana; shetani ameajiri watu wengi na wengine ni marafiki zetu wa karibu mno. **Zab. 55: 12 – 14, Neh. 6: 10 – 13; tusipumbazike,** tutang'olewa macho na kuteswa; kwa sasa adui anashindwa kutufunga na kututesa maana hawezi kututesa tukiwa na ushirika mzuri na Mkuu wa uzima wetu Yesu Kristo. **Tusipumbazike na manabii hawa wengi; tusipumbazike na mifumuko hii mingi ya dini (Madhehebu), tusipumbazike na mifumo mingi ya dunia hii, tusipumbazike na wanasiasa; kila wakati tuwe macho kiroho na kulishika Neno la Mungu wetu usiku na mchana pamoja na kukesha katika sala. Ufun. 3: 7-13. Kama kuna hitaji kubwa sana ambalo wateule wanahitaji kuliomba kwa Mungu kwa bidii na kwa kumaanisha ni hitaji la kupewa karama ya kupambanua roho ili waishi kama Mitume na Manabii waliotutangulia. Matendo 5: 1 – 5, 1Yoh. 4: 1. Amina**

***Na***
***Ask. Dr. L. Mwizarubi***
***August 2021***